JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

---

# TANGAZO

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Geita inatangaza nafasi za kukodi magari kwa shughuli maalumu ya kufanyika kwa mtihani wa darasa la Saba (PSLE – 2025) kuanzia tarehe **09/09/2025 hadi 11/09/2025**.

Mwananchi yeyote mwenye gari/magari anayeweza kufanya kazi hiyo alete maombi kwa kupitia Idara ya Ugavi au Elimu Msingi (W).

**MASHARTI YA MWOMBAJI**

1. Gari lazima liwe na uwezo wa kubeba watu nane (8) na kuendelea na liwe na nafasi ya kupakia mizigo.
2. Gari lazima liwe zima linalofaa kufanya kazi kwenye Barabara za vijijini
3. Dereva lazima awe na leseni hai na mwenye kuzingatia Kanuni za Usalama Barabarani.
4. Gari lazima liwe na kadi ya umiliki, liwe limekatiwa bima, na kifaa cha kuzimia moto.
5. Mmiliki wa gari lazima awe tayari kukaguliwa gari lake na Mkaguzi wa Magari (Vehicle Inspector), kabla ya siku ya Mtihani.

CamScanner

6. Mmiliki /Dereva atatakiwa kufunga mkataba wa kufanya kazi za mtihani siku moja kabla ya siku ya mtihani.

7. Maombi lazima yaambatane na kivuli cha kadi ya gari na kivuli cha leseni ya Dereva.

8. Halmashauri haitahusika na matengenezo yoyote endapo gari litaharibika au kupata ajali kwa kipindi chote cha shughuli za Mtihani

9. Halmashauri haitaweza kumlipa mwenye gari ambaye gari lake litashindwa kufanya kazi aliyopangiwa hata kama atakuwa amefunga mkataba.

10. Malipo yatafanyika baada ya kazi ya mtihani kukamilika.

11. Halmashaurai itatoa **mafuta** kwa kazi yote kulingana na umbali uliopo.

**12.** Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **05.09.2025 saa 9.30 jioni,** na magari yatakayokuwa yamepitishwa yatakaguliwa tarehe **08.09.2025** kuanzia saa 2:15 asubuhi, Eneo la **Ofisi za Zamani za Halmashauri ya Wilaya Geita (Bomani)**

Maombi yatumwe kwa:
Mkurugenl Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Geita,
S.L.PO. 139,
**GEITA.**

**Tangazo limetolewa leo 28.08.2025**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA GEITA

Khashimu Lugome
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**GEITA**

CamScanner